

Mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili Miaka Hamsini Baadaye

Enock Matundura¹, Timothy M. Arege² na John Kobia¹

¹*Chuo Kikuu cha Chuka, Kenya*

²*Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*

Ikisiri

Mnamo miaka ya 1960, kulizuka mgogoro miongoni mwa wataalamu wa Kiswahili kuhusu ushairi wa Kiswahili ambao kimsingi uliochochewa na masuala mawili. Kwanza, utata kuhusu maana ya ushairi kwa jumla na pili, maana ya shairi la Kiswahili. Mgogoro huo ulizua pande au mapote mawili yaliyokinzana. Upande mmoja ulikuwa wa ‘wanamapokeo’ au ‘wahifadhina’ na pote la pili likawa na ‘wanausasa’ au ‘wanamapinduzi’ au ‘wanamabadiliko’. Wanamapokeo walishikilia kwamba uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili ni sheria au arudhi za urari wa vina na mizani, ilihali pote la wanamapinduzi likashikilia kwamba haikuwa lazima shairi la Kiswahili kuwa na urari wa vina na mizani. Wanamabadiliko wanasema kwamba shairi la Kiswahili linaweza kuwa ‘huru’ na si lazima mshairi afungwe na kanuni za sheria au arudhi za vina na mizani anapotunga shairi. Lengo la makala haya ni kuangazia ‘mgogoro’ huu baada ya takriban zaidi ya miaka hamsini (50) tangu ulipozuka ili kutathmini iwapo ulififia au bado ungalipo. Makala haya yamechochewa na hatua ya kuchapishwa kwa diwani za mashairi zinazowaleta pamoja wanamapokeo na wanamapinduzi. Baadhi ya diwani hizo ni pamoja na Tamthilia ya Maisha (Wamitila, Mhar. 2002), Diwani ya Karne Mpya (Walibora, Mhar, 2007), Waja Leo, (Walibora, Mhar. 2012), Tunu ya Ushairi (Arege, Mhar. 2013). Je, hatua hiyo inaashiria nini kuhusu ‘mgogoro’wa ushairi wa Kiswahili wa miaka ya 1960 na 1970?

Maneno Muhimu: *Mgogoro, Wanamapokeo, Wanamapinduzi, Arudhi*

Asili ya Mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili

Mgogoro¹ katika ushairi wa Kiswahili umekuwepo tangu miaka ya 1960. Baada ya mataifa ya Afrika Mashariki kujipatia uhuru, wataalamu na waandishi chipukizi

¹Dhana ya ‘mgogoro’ inamaanisha mawazo yanayokinzana au misimamo inayokinzana baina ya watu wawili au

makundi ya watu. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI)* inafafanua ‘mgogoro’kama hali ya kutoafikiana baina ya

wakati huo, kama vile Jared Angira, Euphrase Kezilahabi, Ebrahim Hussein, Crispin Haule, Mugyabuso Mulokozi, na Kulikoyela Kahigi walianza kuandika tungo zisizokuwa na vina wala urari wa mizani (Njogu na Chimerah, 1998:112). Waliziita tungo hizo ‘Mashairi ya Kisasa’². Tungo hizo zilikuwa tofauti na mashairi ya hapo awali yaliyofuata arudhi³. Utunzi wa tungo ambazo hazikuwa na vina na mizani ulifasiriwa kuwili. Kwanza kuna wale walioichukulia kuwa hatua ya kimaendeleo⁴ huku wengine wakidai kwamba ilikuwa hatua ya kurudi nyuma kisanaa. Aina hii mpya ya mashairi ilisababisha ukosefu wa istilahi⁵ ya kifasihi ya kutajia aina mpya ya kazi ya kisanaa au utanzu ibuka. Watunzi walioanzisha mgogoro huu walikuwa vijana wasomi wenyewe elimu ya vyuo vikuu ambako walikuwa wametagusana na fasihi za maeneo mengine ulimwenguni. Katika mtagusano huo, walibaini kwamba fasihi hizo hazikufuata ruwaza ya vina na mizani. Euphrase Kezilahabi, msomi chipukizi wa wakati huo ambapo mgogoro wa ushairi wa Kiswahili ulianza na ambaye alikuwa ametunga mashairi yasiyofuata arudhi katika diwani yake iitwayo *Kichomianasema*:

[...] wataalamu wetu wa mashairi wamesisitiza mambo madogo madogo ya mashairi. Mambo kama mizani, vina, kituo na kutosheleza ni mambo madogo ya utunzi na si kiini cha shairi au maana ya shairi. Mambo kama haya yamewafanya watu wengi wafiriki kwamba shairi bila mizani au vina si shairi. Mizani na vina hayana maana kama hayakutumiwa vizuri na mshairi ili

pande mbili au zaidi; mkwamo.

²Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi kwa mfano wameipa diwani yao anwani *Mashairi ya Kisasa* (TPH, 1973)

³Dhana hii inamaanisha elimu ya kanuni za utunzi wa ushairi. Taz. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI).

⁴Farouk Topan kwa mfano anasema kwamba, mashairi ya Kezilahabi yanakuza fasihi ya Kiswahili kwa njia mbili.

Njia ya kwanza yahu muundo wa mashairi ya Kiswahili na njia ya pili ni kuvumbua mito mingine ya kishairi

pia na kutufunulia mawazo ya aina fulani ya kisasa. Taz. Dibaji yake katika *Kichomi* (1973: vii-xii).

⁵Mojawapo ya matatizo makuu ya tanzu ni ukosofu wa istilahi za kutajia tanzu na kubadilika kwa tanzu zilizopo. Tanzu mpya zinapozuka, huwa hazina majina yanayokubalika na watu wote. Kwa hiyo, mashairi yaliyokiuka kaida za kimapokezi yalipewa majina tofautitofauti kama vile ‘mashairi huru’, ‘mavue’, ‘mtiririko’, ‘mapingiti’ n.k. Katika utanzu wa riwaya, kuchapishwa kwa tungo mbili za Euphrase Kezilahabi, *Nagona* (1991) na *Mzingile* (1992), wahakiki wengi walishindwa jina la kuziita. Mpaka sasa, wahakiki wengi wa fasihi ya Kiswahili hawajakubaliana iwapo kazi hizi ni riwaya au si riwaya. Mbatiah (2001:7) kwa mfano anazitaja *Nagona* na *Mzingile* kuwa ni ‘Dhidiriwaya’ kwa misingi kwamba zinapuuza kimakusudi na kuvunja kaida za utunzi wa riwaya kama vile uhusika, ploti n.k. Taz. *Kamusi ya Fasihi* (2001). Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

kufanya shairi lake lieleweke vizuri zaidi. Wataalamu wengine wameandika sheria za kutunga mashairi⁶. Hakuna sheria za kutunga. Kila mshairi ana njia yake ya kutoa mawazo yake kishairi. Zile ambazo wataalamu wanaita ‘sheria’ ni yale mambo yanayofanana katikamashairi fulani kwa wakati fulani lakini si sheria. (Kezilahabi, 1977:59-60).

Mawazo ya Kezilahabi yanafumbata misimamo ya wanamapinduzi wenzake wa wakati huo wakiwemo Jared Angira, Euphrase Kezilahabi, Ebrahim Hussein, Crispin Hauli, Mugyabuso Mulokozi, na Kulikoyela Kahigi, F. Senkoro na wengine waliokuja kuukumbatia uanamapinduzi baadaye kama vile Alamin Mazrui, S.A.Mohammed, Kithaka wa Mberia, Kineene wa Mutiso mionganoni mwa wengine. Naye Ibrahim Noor Shariff (1988:183), wa kundi la wanamapokeo⁷ anadai kwamba:

[...]Mzozo ulizuka pale wale wanaojiita ‘wanamabadiliko’walipodai mambo matatu; kwanza, kunena kuwa mbinu za kutunga za Kiswahili ni chache mono, na pili, kuhubiri kuwa kutunga kwa kufuata taratibu za muundo wa tungo za Kiswahili kuliwanyima wao uhuru wa kutunga. Tatu, kudai kuwa muundo wa maandishi yao ni tungo za asili ya Kibantu, kwa hivyo muundo huo ni wa asili ya Kiswahili pia na si ya Kigeni kwa Waswahili. Muundo wa uandishi waliokuwa wakiutetea wanamabadiliko ni ule mtindo wa kuandika maneno bila ya kufuata taratibu zozote zinazokubalika kuwa ni tungo kwa Waswahili: Muundo usiokuwa na mizani, usioteremka kwa , wala usiofuata sauti za mahadhi.

Inabainika wazi kwamba maoni ya Euphrase Kezilahabi ambaye tumementaja kuwa kiwakilishi cha wanamapinduzi yanajibu masuala matatu ambayo Ebrahim Noor Shariff wa pote la wanamapokeo anadai kuwa ndiyo yaliyokuwa chanzo cha mgogoro wa ushairi wa Kiswahili. Je, mgogoro huu ulikuza vipi au kudumaza maendeleo ya utanzu wa ushairi Afrika ya Mashariki? Je, kati ya wanamapinduzi na wanamapokeo, ni lipi lilioshinda kwenye mjadala au mgogoro huo kuhusu ushairi wa Kiswahili? Maswali haya hayawezi kupata majibu kwa urahisi na ya uhakika bila kuangalia mkondo wa uchapishaji wa tungo za mashairi tangu miaka ya 1960 na 1970 wakati ambapo mgogoro huo ulikuwa katika kilele chake.

⁶Kezilahabi anazungumzia *Sheria ya Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* iliyotungwa na Abedi,K.A. (1954) na kuchapishwa na Kenya Literature Bureau, Nairobi.

⁷ Hawa ni watu wa kundi lioamini kwamba urari wa vina na mizani ni roho na uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Wanashikilia kwamba ruwaza za vina na mizani ndizo zinazoufanya ushairi wa Kiswahili ujitalambushe. Wafuasi wa kundi hili ni pamoja na Kaluta Amri Abedi, Abdilatif Abdalla, Shihabbuddin Chiraghdin, Hassan Mwalimu Mbega, Saadan Kandoro, Ahmad Sheikh Nabhan na Jumanne Mayoka, Abel Gibbe, David Massamba mionganoni mwa wengine Wanamapokeo pia wanarejelewa pia kama ‘wahifadhina’ au ‘wahafidhina’ au ‘wanajadi’.

Aidha, mambo mengine yaliyochangia mgogoro wa ushairi wa Kiswahili ni athari za kisiasa. Tulivyotaja ni kwamba, mgogoro huu ulianza miaka michache baada ya mataifa ya Afrika Mashariki kujipatia uhuru wa bendera. Hali hii ilisababisha mivutano ya kijamii. Kulikuwa na mwamko mkuu wa kisiasa na mzinduko. Watu walisaili na kuhojihoji mapokeo yote ikiwemo mipaka iliyowekwa na jamii za kikoloni kama vile mamwinyi na aina za utunzi kwa manufaa yao binafsi. Vilevile mazingira ya kiisimu yalichochea mgogoro wa ushairi wa Kiswahili.

Mkondo wa Uchapishaji wa Diwani za Mashairi Afrika Mashari baada ya Uhuru

Wakati mgogoro wa ushairi ulipoanza, hususan mnamo miaka ya 1960 na 1970, kulikuwa na diwani chache ambazo zilikuwa zimeandikwa kwa kuzingatia arudhi au kanuni zilizopingwa baadaye na wanamapinduzi. Baadhi ya diwani hizo ni pamoja na *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Jinamizi* (Zakwany, 1970), *Mashairi ya Saadani Kandoro* (1972), *Diwani ya Akilimali Snow White* (Akilimali, 1973), *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973), *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri Abedi* (Abedi, 1973), *Malenga wa Mvita* (Nassir, 1974), *Diwani ya Mnyampala* (Mnyampala, 1975), *Umbuji wa Kiwandeo* (Nabhany, 1977) na *Malenga wa Mrima*⁸ (Mwinyihatibu, 1977). Katika kipindi hicho cha miaka ya 1970 vilevile, diwani za wanamapinduzi zilitokea na kuchochaea mgogoro huo. Tungo hizo ni pamoja na *Kichomi* (Kezilahabi, 1973), *Mashairi ya Kisasa* (Mulokozi na Kahigi, 1973), na *Malenga wa Bara* (Mulokozi na Kahigi, 1976). Kati ya watunzi hawa wote katika pote hili, Euphrase Kezilahabi anashikilia nafasi muhimu katika mgogoro wa ushairi kuhusiana na suala la ‘mapinduzi’. Akishadidia hoja hii, Wamitila (2008) anasema:

E.Kezilahabi [...] ni mshairi muhimu sana katika historian a maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Diwani yake ya kwanza, Kichomi, ilipochapishwa katika mwaka wa 1974, kama diwani ya kwanza ya mashairi yasiyofungwa kwenye ‘arudhi’- mashairi yaliyofurahia uhuru wa kisanaa – ambayo ni sifa muhimu ya Sanaa yoyote ile, ilizua timbago kubwa mionganoni mwa ‘wataalamu’ na watunzi ambaeo walizoea kuyavaa magwanda ya umapokeo na kucheza ngoma ya ushairi. Yalibuniwa maneno ya kila aina kuelezea ushairi huo n ahata, wengine kutabiri kifo chake. Shutuma kuu iliyotolewa kuyahuusu mashairi hayo ni kuwa yalitumia lugha ya kawaida na ushairi si wa lugha ya kawaida bali ni wa lugha teule.⁹

Ni muhimu kutaja katika hatua hii kwamba, mgogoro huu wa ushairi ulionekana na kudhihirika katika tungo za wafuasi wa mapote mawili. Kila mwamba ngoma alivutia kwake pindi alipopata fursa ya kuutetea mrengo wake. Tazama anavyosema Chiraghdin katika utangulizi wa mhariri kwenye *Malenga wa Mrima* (1977:3):

⁸Tungo hizi zilihaririwa na Shihabuddin Chiraghdin ambaye ni mwanamapokeo.

⁹Taz. Utangulizi wa K.W. Wamitila katika *Dhifafa* (E.Kezilahabi,2008; uk.v).

[...]Na jambo ambalo lautenga ushairi wa Kiswahili na tungo nyengine za Kiswahili, ni umbo lake. *Shairi wa Kiswahili hukosa umbo lake likikosa vina na mizani*; na hapo huwa haliitwi tena shairi. (Mlazo ni Wetu).

Katika kuwajibu wanamapokeo kuhusu utunzi wa mashairi yaliyofuata sheria au kanuni fulani, wanamapinduzi, wakiongozwa na Euphrase Kezilahabi na Mugyabuso Mulokozi na Kulikoyela Kahigi waliandika utangulizi kwenye kazi zao uliotetea ‘mapinduzi’ yao. Kezilahabi anasema kwenye utangulizi wa *Kichomi* (173:xiii):

Mtu ye yeyote akiniuliza
Kwa nini vina na mizani
Situmii na mistari na
Beti sitoshelezi.
Nitamwaambia: Rafiki
Kuna njia nyingi za kwenda
Bustanini.
Lakini kama mtu yuleyule
Kunisoza akiendelea na kuniambia
Njia niliyotumia ni mbaya,
Nitamwambia:
Rafiki, twende nyumbani kwangu
Kwa mguu, na nyumbani kwangu
Tukifika jaribu kunifunza
Kutembea.

Ni wazi kwamba Kezilahabi anawabeza na kuwasuta wanamapokeo kwa kusema kwamba mtunzi anaweza kutumia lugha ya kawaida; lugha itumiwayo na watu wa kawaida katika mazungumzo yao ya kawaida ya kila siku isiyokuwa na mafumbo jinsi inavyokuwa katika mashairi yanayozingatia vina na mizani. Kwa hivyo, haya ni mapinduzi ya aina nyingine yanayoukomboa ushairi wa Kiswahili ambao kwa muda mrefu ulikuwa mazungumzo kati ya watu wachache au kikundi cha watu wanaouelewa.

Katika *Mashairi ya Kisasa* (1973:vi), Mulokozi na Kahigi wanahalalisha hatua yao ya kutunga tungo zilizokaidi mitindo ya wanamapokeo; ingawa vilevile wanasema kwamba ni dhahiri mtunzi azijue kanuni za ushairi walakini asizichukulie kama kanuni zisizobadilika. Wanasema kwenye Utangulizi:

Hiki ni kitabu cha mashairi na tenzi mbalimbali. Kimeitwa MASHAIRI YA KISASA hasa kwa sababu mitindo iliyotumika humu ni ya aina tofauti kabisa na ile iliyozoewa. Washairi wengi wanazijua na kuzifuata kanuni za mizani, vina na vibwagizo, na kadhalika kama anavyoeleza marahemu Kaluta Amri Abedi katika kitabu chake Sheria za Kutunga Mashairi [...] Walakini ni maoni yetu pia kwamba utunzi wa mashairi hauna budi kubadilikabadilika. Njia nyingine nzuri na mpya hazina budi kuvumbuliwa na watunzi wenye ari ya kuendeleza kipawa chao cha mashairi na lugha ya Kiswahili [...] tumeandika mashairi na tenzi hizi katika mitindo mipyka kabisa bila kutawaliwa sana na kanuni za washairi waliotutangulia.

Mnano miaka ya 1980 na 1990, diwani zaidi za mashairi zilichapishwa. Mkumbo huo wa diwani ni pamoja na *Malenga wa Vumba* (Amana, 1982), *Sikate Tamaa* (Mohamed, 1983), *Chungu Tamu* (Mvungi, 1985), *Kina cha Maisha* (Mohamed, 1986), *Mizani Yangu* (wa Mutiso, 1986), *Chembe cha Moyo* (Mazrui, 1988), *Malenga wa Ziwa Kuu* (Wallah, 1988), *Fungate ya Uhuru* (Khatib, 1988), *Kimbunga* (Haji, 1994) na *Mchezo wa Karata* (Mberia, 1997) mionganoni mwa tungo nyininge. Kutokana na orodha hii ya baadhi ya diwani za mashairi zilizochapishwa katika miaka ya 1980 na 1990, inabainika kwamba wanamapokeo waliendelea kutunga mashairi yaliyozingatia vina na mizani, huku wanamapinduzi kama vile Alamin Mazrui wakitunga mashairi yaliyokiuka kanuni za utunzi.

Hata hivyo, katika miaka ya 2000, mbali na kuchapishwa kwa diwani za wanamapinduzi kama vile *Bara Jingine* (Mberia, 2001) na *Jicho la Ndani* (Mohamed, 2002), Dhifa (Kezilahabi, 2008), uchapishaji wa diwani za mashairi ya Kiswahili ulichukua mkondo tofauti na ule uliozoeleka. Tathmini ya jicho kali inaonesha kwamba, katika kipindi kizima cha mgogoro wa ushairi wa Kiswahili, wanamapokeo walijitenga na kutunga diwani zao zilizozingatia arudhi za utunzi wa mashairi. Wanamapinduzi nao walitunga diwani zao kando ambazo zilikuwa na mashairi yasiyozingatia arudhi. Hatua hiyo inaweza kuelezewa kama labda mbinu ya kutetea misimamo mikali ya kila pote kuhusiana na suala zima la ‘mgogoro wa ushairi wa Kiswahili’. Mkondo tofauti tunaouzungumzia katika makala haya ni ule wa wasomi wa fasihii ya Kiswahili kuanza kukusanya mashairi ya wanamapokeo na wanamapinduzi na kuyachapisha pamoja kwenye diwani. Wasomi hao wa fasihii ya Kiswahili (ambao pia ni washairi) ni pamoja na K.W. Wamitila, Ken Walibora na Timothy M. Arege. Tungo za aina hii zilizohaririwa na wasomi hawa ni pamoja na *Tamthilia ya Maisha* (Wamitila, Mhar. 2002), *Diwani ya Karne Mpya* (Walibora, Mhar, 2007), *Waja Leo*, (Walibora, Mhar. 2012), *Tunu ya Ushairi* (Arege, Mhar. 2013).

Katika *Diwani ya Karne Mpya* (Walibora, Mha, 2007) amehusisha mashairi ya wanamapokeo kama vile Abdilatif Abdalla¹⁰, Shaaban bin Robert¹¹ na Ali Salim Zakwany¹². Baadhi ya wanamapinduzi maarufu ambao mashairi yao yameshirikishwa kwenye diwani hii ni pamoja na Alamin Mazrui¹³, Euphrase Kezilahabi¹⁴ na Kineene

¹⁰Tazama mashairi, ‘Kumekucha’ (uk. 24), ‘Kuno Kunena’ (uk.34), ‘Mwerevu Hajinyowi’ (uk.47), ‘Kibaruwa’ (uk.93) na ‘Moyo Iwa na Subira’ (uk. 133).

¹¹ Tazama mashairi, ‘Rafiki’ (uk.59), na ‘Ni Wapuzi’ (uk.126) na ‘Nilinde’ (uk.130).

¹² Tazama mashairi, ‘Kila Mtu Ale Chake’ (uk.26), ‘Ni Makosa Yangu’ (uk.74).

¹³ Tazama mashairi, ‘Niguse’ (uk.28), ‘Kilio cha Afrika’ (uk.36), ‘Hisia’ (uk.73), na ‘Pingu za Utamaduni’ (uk.114)

¹⁴Tazama mashairi, ‘Kisima’ (uk.96), ‘Moshi Ukizidi Pangoni’ (uk.104), ‘Kifo cha Mende Wekundu’ (uk.107) na ‘Ngoma Kimya’ (uk.112)

wa Mutiso.¹⁵ Mhariri wa *Diwani ya Karne Mpya*, Ken Walibora anajaribu kuhalalisha sababu ya kuwaleta pamoja washairi wakongwe na chipukizi kwa kusema:

Ni muhimu kutambua kwamba enzi ya ushairi wa *Kiswahili kuwa milki ya Waswahili pekee imepita*. *Maenezi mapana ya Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki na pembe mbalimbali duniani yamekifanya kuwa lugha ya kimataifa*. Kama vile lugha nyingine za kimataifa (kwa mfano Kiingereza, Kifaransa, na Kihispania), Kiswahili kimetaifishwa na kumataifishwa kiasi kwamba watu wasiokuwa wazawa wa Uswhilini au mwambao wa pwani wameivalia njuga fani ya ushairi wake kwa viwango tofautitofauti. Kwa maneno mengine watu wa asili mbalimbali wameivulia nguo bahari ya utunzi wa mashairi kwa kutumia Kiswahili kama nyenzo ya kubeba hisia zao, mihemko yao ba mawazo yao.

Kauli hii kwa namna moja au nyingine inaakisi mwangwi wa mgogoro wa ushairi wa Kiswahili kwa misingi kwamba, mojawapo ya sababu walizotoa wanamapokeo kupinga mkondo wa mapinduzi katika ushairi wa Kiswahili ni kwamba, kuacha arudhi ni kuharibu utamaduni wa Kiswahili. Wanamapinduzi, ambao wengi wao hawakuwa Waswahili asilia walianza kutunga mashairi katika mazingira na utamaduni tofauti. Kwa hivyo, hawakutaka ushairi ufungwe na minyororo ya arudhi. Kiswahili hakikuwa hakikuwa cha watu wa pwani pekee mazingira ya pwani.

Mataifa ya Afrika ya Mashariki yalipopata uhuru, elimu katika viwango mbalimbali pia ilipanuka. Baadhi ya wasomi walipata fursa ya kusomea fasihi linganishi katika viwango vya juu. Hali hiyo iliwapa fursa ya kudadisidadi na kuhojihoji maswala ya kifasihi kitaaluma ikiwemo ushairi wa Kiswahili. Udadisi huu iliwapa utambuzi kwamba maendeleo katika Sanaa huenda sambamba na maendeleo ya asasi nyinginezo katika jamii. Yaani, fasihi kwa kiwango kikubwa huakisi yale yanayoendelea katika jamii kwa mujibu wa wakati. Aidha, mivutano kama hiyo ilikuwa imetokea katika mataifa ya Ulaya hapo awali. Kuhusu suala la mgogoro wa ushairi wa Kiswahili na usomi, Syambo na Mazrui (1992:46) wanasema:

Lakini hivi karibuni, kumezuka washairi wanaotumia mtindo mpya unaoitwa sukui na tungo-mtiririko. Sukui ni yale mashairi ya kisiku hizi yasiyokuwa na vina lakini yanayofuata mizani, na tungo-mtiririko au mavue ni yale yasiyokuwa na vina wala mizani. Mashairi ya aina hii pengine yalianza na wasomi fulani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ingawa sasa yameenea kwingineko. Katika kundi hili pengine tunaweza kuwatia watanzi kama Kezilahabi, Hussein, Mulokozi na Kahigi wa Tanzania, na Mutiso na Mberia wa Kenya. Na bila ya shaka siku za usoni ushairi wa Kiswahili utaendelea kuzaa mitindo mipyä kutokana na sababu na athari mbalimbali.

¹⁵Tazama mashairi, ‘Amani’ (uk.118) na ’Hofu za Bin-Adamu’ (uk.130)

Ingawa Mazrui na Syambo wanatoa kauli yao kwa kuonesha shaka ya ‘pengine’, ni kweli kwamba wanamapinduzi wengi waliwahi kusomea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wataalamu hao walibuka kuwa wahakiki na waandishi hodari waliokuja kuchangia maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Euphrase Kezilahabi kwa mfano hakuchangia katika kuleta mageuzi katika ushairi wa Kiswahili tu bali pia katika utanzu wa riwaya ambapo alitunga riwaya za kimajaribio.¹⁶

Nayo diwani ya *Tunu ya Ushairi* (Arege, Mhar.2013) imewaleta pamoja watunzi wa mashairi ya Kiswahili wanaotunga kwa kufuata arudhi za wanamapokeo na wale wanaotunga bila kuzingatia arudhi hizo. Katika diwani hii yenye mashairi ya watunzi wanne, mshairi mkongwe wa pekee ambaye mashairi yake yameshirikishwa katika kazi hii ni Amiri S. Andanenga.¹⁷ Watunzi wengine chipukizi katika diwani hii kama vile Mwalaa Mranga Nyanje wana uwezo wa kutunga mashairi huru¹⁸ na mashairi yanayozingatia arudhi.¹⁹ Mtunzi Timothy Arege vilevile ana uwezo wa kutunga mashairi yanayozingatia arudhi na yale yasiyozingatia arudhi. Joseph Kiponda vilevile ana uwezo wa kutunga mashairi yanayozingatia arudhi nay ale yasiyozingatia arudhi. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kwamba mashairi yao ya arudhi na yale yasiyokuwa na arudhi yamefinyangwa kwa namna fulani ili kukidhi matakwa ya mshairi. Mhariri wa diwani ya *Tunu ya Ushairi* anasema kwenye dibaji (uk.vii):

Kufikia hii leo, ushairi wa Kiswahili umepitia hatua mbalimbali za maendeleo. Kuna mitindo ya wawali awali zaidi yenye kujikita katika kanuni za kiarudhi na kuna mitindo ya baadaye ya washairi kuzivua kanuni hizo. Tofauti hizi za kimitindo zilizaa kile kilicho julikana kama mgogoro wa ushairi katika miaka ya sitini na sabini. Ingawa sasa vumbi la mvutano huo limetua, bado kuna vuguvugu la mbegu za joto la mvutano huo. Na kama wasemavyo Waswahili, Kila mwamba ngoma huvutia kwake.

Arege anaonekana kuashiria kwamba bado mwangwi wa mgogoro wa ushairi ungalipo miaka zaidi ya miaka hamsini tangu ulipozuka. Kauli hii inatuchochaea kusema kwamba athari za mgogoro wa ushairi zitaendelea kufinyanga mikabala ya uendelezaji wa utanzu wa ushairi wa Kiswahili Afrika ya Mashariki. Ingawa diwani hii imemshirikisha mwanamapokeo mmoja tu, tunaweza kusema kwamba hatua hiyo ni ishara kwamba wanamapokeo na wanamapinduzi hawana budi kushirikiana ili kupiga

¹⁶ Rejelea riwaya zake za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1992)

¹⁷ Amiri S. Andanenga ni mshairi mkongwe wa Kiswahili nichini Tanzania. Mzee Andanenga ni mtunzi wa mashairi ya arudhi. Taz. taarifa za mhariri kuwalhusu wachangiaji wa mashairi kwenye diwani ya Tunu ya Ushairi (uk.184).

¹⁸ Tazama baadhi ya mashairi yake, ‘Ndani ya Nafsi’ (uk.7), ‘Sikati Tamaa’ (uk.21) na ‘Siondoki’ (uk.87)

¹⁹ Tazama baadhi ya mashairi yake, ‘Pambo la Lugha’ (uk.85), na ‘Tusitete’ (uk.115)

makasia pamoja katika safari ya kukuza utanzu wa ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, Arege (keshatajwa) anaendelea kusema:

[...] inapozuka diwani hii, ni zaidi ya miongo mitano tangu uzuke mgogoro wa ushairi wa Kiswahili. Aina zote za ushairi zimeshudia mabadiliko mengi. Mabadiliko haya yanaonesha kuwa sanaa huchukua mikondo mipyka kila uchao, lakini bila kujitenga na nduni zake. Tunu ya Ushairi inaufungua ukurasa mpya unaoonesha mitindo na mikondo mbalimbali iliyotumiwa na washairi wa Kiswahili. Upya huu unatufanya kukubali kuwa dhana mbalimbali za ushairi zinafaa kubadilishwa na kupanuliwa kulingana na hali na viwango vya ubunifu katika ushairi.

Tunakubaliana na Arege kwamba mumo kwa mumo katika mitindo na miundo ya ushairi wa Kiswahili wanaotunga kwa kuzingatia arudhi na wanaotunga bila arudhi panahitajika kupanua bahari za ushairi zilizozoleka na kuzua bahari nyingine mpya.

Nayo diwani ya *Waja Leo* (Walibora, Mhar.2012) imewaleta pamoja washairi kumi (10) kutoka Kenya na Tanzania wanaotunga kwa mikabala ya uanamapokeo na uanamapinduzi. Wengi wao ni waandishi chipukizi. Watunzi hao ni kama vile Pauline Kea, Hamisi Babusa , Omar Babu (Abu Marjan), Ann Samba, Ludovick Mbogholi, Hassan Muchai, Emily Ondeko, Jamal Mutua na Ken Walibora (wote kutoka Kenya) na Mohammed Khelef Ghassany (Zanzibar). Ingawa diwani hii hajjawashirikisha tungo za watunzi wakongwe. Diwani hii vilevile inasheheni mwangwi wa mgogoro wa ushairi wa Kiswahili pale mhariri anaposema kwenye dibaji:

Washairi hawakuwekewa shokoa kutunga ama kwa kuzingatia sheria za mashairi ya arudhi au kuzipuza na kuandika mashairi huru. Aidha, hawakutunga kuhusu mada walizofanyiwa msukumo watunge. Wametunga tu kama akili zao zilivyowaandisi. Kwa raha zao. (Mlazo ni Wetu)

Kutokana na kauli hii inabainika kwamba mgogoro wa ushairi wa Kiswahili bado ni kitovu cha kurejelewa na watunzi wa ushairi wa Kiswahili; hasa katika kufanya maamuzi kuhusu mrengo wa kuegemea katika utunzi wa mashairi. Kuna waandishi chipukizi wa mashairi ya Kiswahili ambao tangu hapo mwanzo wamejinasibisha na pote la wanamapokeo. Mshairi Omar Babu²⁰ ambaye mashairi yake yametokea katika diwani za *Tamthilia ya Maisha* (Wamitila, Mhar. 2002), *Diwani ya Karne Mpya* (Walibora, Mhar, 2007), *Waja Leo*, (Walibora, Mhar. 2012) ni mmoja wa watunzi chipukizi waliojinasibisha na pote la wanamapokeo. Mashairi yake yote ni ya arudhi.

²⁰Omar Babu (Abu Marjan) alikuwa mhadhiri wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Cologne, nchini Ujerumani. Alifariki dunia Januari 19, 2015.

Hitimisho

Katika makala haya, tumeangalia asili ya mgogoro wa ushairi wa Kiswahili na baadhi ya kauli zilizotolewa na mapote mawili; wanamapokeo na wanamapinduzi- kuunga mkono au kuhalalisha misimamo yao. Kadhalika, makala yameangazia mikondo ya uchapishaji wa diwani za ushairi wa Kiswahili tangu mgogoro wa ushairi ulipoanza miaka michache baada ya mataifa ya Afrika Mashariki kujipatia uhuru wa bendera hadi miaka ya 2000. Makala pia yamebaini kwamba watanzi wa baadaye wa diwani za mashairi ya Kiswahili hasa katika kipindi cha miaka ya 2000 kuendelea, walichukua hatua za kimakusudi za kuwaleta pamoja wanamapokeo na wanamapinduzi. Licha ya hatua hiyo, mwangwi wa mgogoro wa ushairi wa Kiswahili bado ungalipo. Aghalabu tungo tulizozirejelea katika makala haya zinataja kwa njia moja au nyingine mgogoro wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, tunaweza kusema kwamba hakuna mshindi wala mshinde katika mgogoro wa Kiswahili. Kuja pamoja kwa watanzi wa mapote haya mawili kwa maoni yetu ni utambuzi wa ukweli tunaoufahamu kama wahakiki kwamba sanaa haiwezi kufungika katika kaida kwa kuwa kaida hubadilika. Vivyo hivyo, hatuwezi kutapia kupya na kusahau kukongwe. Kwa hiyo, mgogoro wa ushairi wa Kiswahili, licha kwamba haujitokezi na kubainika bayana miaka hamsini baadaye, utaendelea kuathiri kwa kipindi kirefu jinsi au namna utanzu wa ushairi unavyotazamwa na wahakiki.

Marejeleo

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abedi, A.K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi: Oxford University Press.
- Arege, T. (2013). *Tunu ya Ushairi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Chiraghdin, S. (mha.) (1977). *Malenga wa Mrima: Tungo za Mwinyihatibu Mohamed*. Nairobi: Oxford University Press.
- Haji, G.H. (1994). *Kimbunga*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kezilahabi, E. (2008). *Dhifa*. Nairobi: Vide-Muwa
- Kezilahabi, E. (1977). ‘Mashairi ya Kiswahili’ Katika *Uchambuzi wa Maandishi ya Kswahili Kitabu cha Pili*. Farouk, M. Topan (mha.) Nairobi: Oxford University Press.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
- Khatib, M.S. (2003). *Wasakatonge*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Mazrui, A. & Syambo, B. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.
- Mberia, K. (1997). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Mberia, K. (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Mnyampala, M. E. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mohamed, S.A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S.A. (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S.A. (1984). *Kina cha Maisha*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mulokozi, M.M., & Sengo, T.S.Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry A.D. 1000–2000*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. & Kahigi, K. (1973). *Mashairi ya Kisasa*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Ltd.
- Nabhany, S.A. (1985). *Umbuji wa Kiwandeo*. Mhariri: Ibrahim Noor Shariff. Nairobi: East African Publishing House.
- Nassir, A.J.B. (1971). *Malenga wa Mvita*: Diwani ya Ustadh Bhalo. Mhariri: Shihabuddin Chiraghdin. Nairobi: Oxford University Press.

- Njogu, K. & Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa Fasihii: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JKF.
- Robert, S. (1972). *Diwani ya Shaaban: Sanaa ya Ushairi*. Nairobi: Thomas Nelson and Sons Ltd.
- Shariff, N. I. (1988). *Tungo Zetu*. New Jersey: The Red Sea Press Inc.
- Walibora, K. (mha.) (2007). *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Walibora, K. (mha.). *Waja Leo*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wamitila, K. W. (2016). *Kichocheo cha Ushairi: Mwongozo wa Uchambuzi wa Mashairi*. Nairobi: Vide-Muwa.
- Wa Mutiso, K. (1986). *Mizani Yangu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.